MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY

# MAISHA

# YA

# TOBA

## SHUKRANI

Namshukuru Yesu kwa kuniwezesha kutoa toleo hili la kwanza la kitabu cha MAISHA YA TOBA. Kitabu hiki namtolea Yesu na Baba yake mapenzi yake yatimie kwa walioitwa na Yesu kuwa wahubiri. Awanurukishie akili zao zipate uelewa au ufahamu juu ya kusudi lake ktk maisha yao. Asante Baba wa Yesu na Yesu pia. Amen.

**MHUBIRIWA KIMATAIFA MINISTRY, FIRST EDITION 2024**

ISBN: 1986 - 08 - 08 - 01

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki hakiruhusiwi ku-nakili, kutafsiri au kuchapishwa kwa njia yoyote bila ru-husa ya Mhubiri wa Kimataifa ministry au Mhubiri wa Kimataifa Lameck Lister. Nakuu zote zimetoka ktk bib-lia (Maandiko matakatifu in Swahili Union Version)

**MHUBIRI WA KIMATAIFA MINISTRY.**

ADDRESS: S.L.P 9332, DAR ES SALAAM

TANZANIA (EFATHA)

MOBILE: +255658601034

EMAIL: listlameck5@gmail.com

MAISHA YA TOBA.

1.Kutubu…………………………………………………………….

2. Hukumu………………………………………………………….

3. Mema……………………………………………………………

4. Aliyeokoka aweza kukosa?Afanyeje  akikosa?……

5. Amri za Mungu……………………………………………….

6. Rushwa…………………………………………………………..

7. Zinaa……………………………………………………………

8. Anasa……………………………………………………………

9.Ulafi……………………………………………………………….

10.Kuokoka………………………………………………………….

11. Mwisho…………………………………………………………

1. KUTUBU

Kutubu ni kumgeukia mungu kuacha kuwa shingo ngumu.Kutubu ni kuacha kutenda dhambi na kutenda haki. Kutubu ni kuacha kutenda mabaya na kutenda mema. Kutubu ni kuacha kutenda tendo lisilotokana neno la kinywa cha Yesu.

**Mathayo 3.2**

**"Tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia. "**

Kutubu ni sehemu ya habari njema iliyohubiriwa na Yesu kwa maskini na wenye dhambi. Kutubu ni sehemu ya wokov u wa mtu aliyeokoka ewe mtu wa kimataifa uliyeokoka sikia hilo ni upate ufahamu ukikosa usihofu kutubu ikiwa si kawaida yako kukosa ktk hilo ulilokosa.

**Ayubu 42:6**

**" Kwa sababu hiyo najichukia nafsi yangu, na kutubu Katika mavumbi na majivu. "**

Kutubu kuna gharama kufunga,kutokula chakula cha anasa na kuvaa magunia na kuketi ktk mavumbi na majivu ,maombi ya rehema au msamaha juu ya dhambi unayoitubia au unazozitubia mbele za mungu ulizoamua kuacha.

Kuokoka ni kutubu, kubatizwa kama Yesu na kujazwa roho mtakatifu.ukweli huwezi kuokoka bila kutubu dhambi na maovu yako mbele za Baba yake Yesu ambaye ndiye mungu kwa jina la Yesu.

## 2.KUTUBU

Maisha uliyokuwa unaishi kabla hujaokoka ni maisha ya maisha ya dhambi tena unazifahamu pengine kuiba, rushwa,kutoshika sabato. Ulipookoko ni kipengele cha kutubu pekee kunafanya kuacha dhambi bali usizozifahamu huondolewa na mungu kwa rehema au huruma zake.

Unaacha maisha ya dhambi maisha ya kale mf: maisha ya ulevi,uzinzi,uongo dhuluma,rushwa na ya amri za Yesu. Na kuishi maisha ya haki mf: maombi, kumwabudu Yesu, kuhubiri au kushuhudia, utoaji,maisha ya kushika amri za Yesu na maagizo yake yanaitwa maisha mapya yaliyo ya haki.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ukikosa tubu usirudie kosa maana Baba wa mbinguni humpenda yeye anajirebisha pale unafahamu ili kosa.

Huu ni wokovu na wewe kama mwana mbele za Baba yake Yesu iko fimbo na lipo gongo ukiendelea kukosa hashindwi kukupiga usidumu ktk kosa penda kuomba msaada wake.

**Zab 23:4**

Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, Sitaogopa mabaya; Kwa maana Wewe upo pamoja nami, <u>Gongo</u> lako na <u>fimbo</u> yako vyanifariji.

Mungu hashindi kukurudi,kukemea na kukuonya kama mwana Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka Mungu aweza kukupiga kwa ugonjwa, kutokufananikiwa, kwa ugonjwa wakati mwingine ukienda hawalioni tatizo lako kutokana na kuacha kutokwenda kanisani kwa muda mrefu kidogo na huna sababu ya msingi (wokovu) au kukuoseka kipato nyumbani kutokana na kutotoa zaka au fungu la kumi.Ni mifano ya fimbo kutoka kwa mungu kwa wafanyakazi au mfanyabiashara .

## 3. HUKUMU

Hukumu ni adhabu inayotokana na kushitakiwa kwa makosa yaliyoshuhudiwa mashahidi mbele za hakimu.

**Math 11:20-22**

“Ndipo akaanza kuikemea miji ile ambamo ndani yake ilifanyika miujiza yake iliyo mingi, kwa sababu **haikutubu.**

Ole wako, Korazini! Ole wako, Bethsaida! Kwa kuwa kama miujiza iliyofanyika kwenu ingalifanyika katika Tiro na Sidoni, wangalitubu zamani kwa kuvaa magunia na majivu.

Walakini nawaambieni, itakuwa rahisi Tiro na Sidoni kustahimili **adhabu** zao siku ya **hukumu** kuliko ninyi. “

Kutokutubu na kudumu ktk dhambi ya kutokumwamini Yesu na Amri zake na maagizo yake ukifa bila kutubu kuna adhabu inayotakana hukumu.ya dhambi zako mojawapo kutokumwamini Yesu.

**Luk 16:19-31**

**“...**Ikawa yule **maskini alikufa,** akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa, akazikwa.

Basi, kule kuzimu aliyainua macho yake, alipokuwa katika mateso, akamwona Ibrahimu kwa mbali, na **Lazaro** kifuani mwake.

Akalia, akasema, Ee baba Ibrahimu, nihurumie, umtume Lazaro achovye ncha ya kidole chake majini, auburudishe ulimi wangu; kwa sababu ninateswa katika **moto** huu.... **“**

Huu ndio ukweli ukimkataa kumwamini Yesu na Kumfuata ktk maisha ya duniani na kudumu ktk dhambi unaishia ktk moto. Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka mshike Yesu dumu ktk imani yake na umfuate kwa uaminifu siku zote za maisha yako ya wokovu utafika mbinguni kama Lazaro.

## 4. HUKUMU

### Luk 13:1-5

**13.1** Na wakati uo huo walikuwapo watu waliompasha habari ya Wagalilaya wale ambao Pilato alichanganya damu yao na dhabihu zao.

**13.2** Akawajibu akawaambia, Je! Mwadhani ya kwamba Wagalilaya hao walikuwa wenye dhambi kuliko Wagalilaya wote, hata wakapatwa na mambo hayo?

**13.3** Nawaambia, Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.

**13.4** Au wale kumi na wanane, walioangukiwa na mnara huko Siloamu, ukawaua, mwadhani ya kwamba wao walikuwa wakosaji kuliko watu wote waliokaa Yerusalemu?

**13.5** Nawaambia, Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo.

Yapo maangamizi yanayoweza kupata mtu kwa sababu ya kukataa kutubu baada ya kuifahamu ile kweli kwa kuhubiriwa na watumishi wa mungu ni yale anahubiriwa ni maisha ya dhambi na anafahamu yana maangamizi ili hataki kubadilika.Ee mtu wa kimataifa mojawapo ya faida ya Toba kukuokoa na maangamizi usiyotarajia kama ajali.

**Zab 103:3**

3. Akusamehe maovu yako yote, Akuponya magonjwa yako yote,

Baadhi ya magonjwa yanatokana na maovu. Tabia ya kutubu itakuokoa na magonjwa pale tu unapofanya kosa kwa mara kwanza na mara moja kutubu papo hapo na kukataa kuendelea kutenda hilo kosa.

## 4. MEMA

Maisha ya Toba  ni maisha ya kutenda mema, ni maisha kuacha baya ulilokuwa ukilitenda na kutenda kinyume cha hilo baya. Mf: ulikuwa mlevi baada **kuokoka**(**kutubu** +ubatizo+roho mtatifu) unatakiwa uombe ujae roho mtakatifu kila siku kipimo cha Yesu kadri moyo wako unavyoweza kubeba na ulivyokusudiwa na Mungu umtumikieje? ( Ulevi ==>**kuokoka**==> Roho mtakatifu).

**Luk 3.3  - 14**

"Akafika nchi yote iliyo karibu na Yordani, akihubiri ubatizo wa toba liletalo ondoleo la dhambi, "Makutano wakamwuliza, Tufanye nini basi? Akawajibu akiwaambia, Mwenye kanzu mbili na ampe asiye na kanzu; na mwenye vyakula na afanye vivyo hivyo. Watoza ushuru nao wakaja kubatizwa, wakamwuliza, Mwalimu, tufanye nini sisi?  Akawaambia, Msitoze kitu zaidi kuliko mlivyoamriwa.  Askari nao wakamwuliza, wakisema, Sisi nasi tufanye nini? Akawaambia, Msidhulumu mtu, wala msishitaki kwa uongo; tena mtoshewe na mshahara wenu. "

Baada ya kutubu ee mtu wa kimataifa uliyeokoka mungu anataka akuone ukitenda mema na kuyatafuta kumwonyesha Mungu wako umebadilika ktk maandiko hapo juu askari mwenye dhambi ya kudhulumu  mungu anataka kuona humdhulumu na unatosheka na msharaha ikiwa unasema hautoshi mwombe mungu akupe akili kwa mshahara huo ufanyeje ili upate ule unaukutosha bila kudhulumu uwe uvumilivu dumu ktk kutodhurumu mtu kipindi chote cha mshahara ambao kwa mshahara hautoshi mpaka mungu atakapokupa akili.

Ukitubu ukiwa mwema mfano ulikuwa na tabia ya kusema uongo jifunze kusema kweli,ulikuwa,ulikuwa mzinzi tosheka na mkeo  na

mzidi farisayo kwa haki ya kufunga kwa juma anayefunga mara mbili ktk siku saba za juma.Saidia watoto wa mitaani na wajane ktk vituo vyao walau mara moja kwa mwaka.shuhudia/hubiri injili kwa wagonjwa na wafungwa unaenda kuwaona kama Yesu alivyosema usisahau kuwaombea wanaoikubali injili.

**Luk 6.35** “Bali wapendeni adui zenu, tendeni mema, na kukopesha msitumaini kupata malipo, na thawabu yenu itakuwa nyingi; nanyi mtakuwa wana wa Aliye juu, kwa kuwa yeye ni mwema kwa wasiomshukuru, na waovu. “

**Marko 10.17—18** “Hata alipokuwa akitoka kwenda njiani, mtu mmoja akaja mbio, akampigia magoti, akamwuliza, Mwalimu mwema, nifanye nini nipate kuurithi uzima wa milele?

Yesu akamwambia, Kwa nini kuniita mwema? Hakuna aliye mwema ila mmoja, ndiye Mungu. “

Mwema ni mungu peke yake ambaye ni Baba yake Yesu wa mbinguni. Ukitafuta kuwa mwema hutafuta kufanana Mungu maana wema ni asili yake. Ni mojawapo za tabia za wana wa mungu yaani waliokoka mungu anataka akuone unakuwa nayo hata ile kushuhudia ee mtu wa kimataifa mungu akikutendea mema usiache kushuhudia kanisani na rafiki au jamaa Mf: wa matendo mema ya mungu anayoweza kukutendea kukubariki,kukuponya na kukutendea miujiza , kukutajirisha kama mfalme sulemani n.k

**Mathayo 5.45** ili mpate kuwa wana wa Baba yenu aliye mbinguni; maana yeye huwaangazia jua lake waovu na **wema,** huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. **Math12.12** - 13 “...Basi ni halali kutenda **mema** siku ya sabato. Kisha akamwambia yule mtu, Nyosha mkono wako; akaunyosha**, ukapona**, ukawa mzima kama wa pili.

## 6. ALIYEOKOKA AWEZA KUKOSA? AKIKOSA AFANYEJE?

**1 kor 6 : 1-20** <u>ALIYEOKOKA AWEZA KUKOSA?</u>

“Bali mwashitakiana,**ndugu** kwa ndugu, tena mbele yao wasioamini.”

**Ndugu** ktk andiko hapo juu ni waliokoka kama wewe mtu wa kimataifa uliyeokoka wanaweza kufanya makosa ukitaka kuelewa zaidi Ukweli soma **1 kor 6** yote.

Tena umwonapo nduguyo akitenda dhambi isiyo ya mauti mwombee mbele za Baba wa mbingu na ukikosa tubu haraka roho mtakatifu hakai na dhambi.

**1 Yoh 5.16**

“Mtu akimwona ndugu yake anatenda **dhambi** isiyo ya mauti, **ataomba,** na Mungu atampa uzima kwa ajili ya hao watendao dhambi isiyo ya mauti. Iko dhambi iliyo ya mauti. Sisemi ya kwamba ataomba kwa ajili ya hiyo. “

Kwa uthibitisho mtu aliyeokoka aweza kukosea au kutenda dhambi ila akijifahamu anatakiwa atubu na ndugu ukimwona anakosa muombee msamaha au rehema mbele za Baba wa mbinguni na kumwonya kwa upole bila kumkwaza.

**Math 18.15—17**

“Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo.

La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike.

Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru. “

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ndugu aliyeokoka mwenzako akikusea mwonye kama mara mbili ila ya tatu liambie kanisa.

## 7. ALIYEOKOKA AWEZA KUKOSA? AKIKOSA AFANYEJE?

Ukitafakari **1 Yoh 5:16** na **Math 18.15—17**

**1 Yoh 5.16** AKIKOSA AFANYEJE?

"Mtu akimwona ndugu yake anatenda **dhambi** isiyo ya mauti, **ataomba,** na Mungu atampa uzima kwa ajili ya hao watendao dhambi isiyo ya mauti. Iko dhambi iliyo ya mauti. Sisemi ya kwamba ataomba kwa ajili ya hiyo. "

**Math 18.15—17**

"Na ndugu yako akikukosa, enenda ukamwonye, wewe na yeye peke yenu; akikusikia, umempata nduguyo.

La, kama hasikii, chukua pamoja nawe tena mtu mmoja au wawili, ili kwa vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno lithibitike.

Na asipowasikiliza wao, liambie kanisa; na asipolisikiliza kanisa pia, na awe kwako kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru. "

AKIKOSA AFANYEJE?

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ukikosa au ukitenda dhambi unapaswa **kutubu** na **kuomba** usirudie lile kosa au dhambi hivyo jinsi ya kufafanya unapokosa.

Ktk kanisa la waliokoka rafikiyo ndugu aliyeokoka kama wewe akikosa au kutenda dhambi isiyo ya mauti mwombee mbele za mungu msamaha au rehema nenda ukae na kumwonya juu ya kosa lake au dhambi anayotenda kama mara mbili akibadilika na kuacha mshukuru mungu umempata nduguyo asipobadilika liambie kanisa.

Mambo mawili ya kuzingatia ukikosa au kutenda dhambi isiyo ya mauti ni ee mtu wa kimataifa uliyeokoka usizoelee makosa au dhambi ktk wokovu wako kama ilivyokuwa ktk dini ulizotokea ni:

1**) Kutubu**2)**Kuomba** uyaweke moyoni yatalinda ushirika wako& Yesu

## 8. AMRI ZA MUNGU

Kaushik amri za mungu kwa kuzitenda alizopewa nabii Musa ktk mlima Sinai ni sehemu ya maisha ya toba. Ewe mtu wa kimataifa uliyeokoka maisha ya toba yapok ndani ya wokovu ni sehemu yako unapaswa kuyaishi. Ukiokoka umekubaliana na hayo maisha ya toba hivyo kuzitenda amri za Mungu kami usage na useable na zinginezo ni sehemu ya maisha yako ya Toba. Amri za mungu unaweza kuzisoma ktk biblia kitabu.

**Kutoka 5 : 1—21**

"...16 Waheshimu baba yako na mama yako; kama Bwana, Mungu wako, alivyokuamuru, siku zako zipate kunzite, nawe upate kufanikiwa katakana nchi upewayo na Bwana, Mungu wako.

17 Usiue.

18 Wala usizini.

19 Wala usiibe.

20 Wala usimshuhudie jirani yako uongo.

21 Wala usimtamani mke wa jirani yako; wala usiitamani nyumba ya jirani yako, wala shamba lake, wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala kitu cho chote alicho nacho jirani yako. "

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka ukishika amri za mungu wewe ni mcha mungu hupendwa na Mungu na Yesu mwanaye.Amri za mungu zinakusaidia kujichunguza kama kuna uovu wowote umeutenda ktk siku upate kutubia kabla kuomba. Yesu alisema yatosha siku na maovu yake.ktk wokovu wako kila siku muda wa maombi yako binafsi usiku au jioni kujikagua kwa kutumia amri za mungu kama umetenda maovu utubu na kujitakasa. Ukizishika amri za unamwosha mungu moyo wako unampenda si maneno ya kinywa tu.

## 9. AMRI ZA MUNGU

**Mathayo 6.33 – 34**

“Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.

Basi msisumbukie ya kesho; kwa kuwa kesho itajisumbukia yeny ewe. Yatosha kwa **siku maovu** yako” .

Ktk biblia ukweli wa wachamungu yaani wazishikao amri za mungu mungu aliwapa mali walikuwa watoaji wazuri wa matoleo na sadaka wengine walikuwa wema mfano Ibrahimu,Ayubu na Kornelio. Kumcha bwana au kuzishika amri za mungu ni tunda la kutubu na kuuzoeza mwili kutenda amri za mungu.

**Matendo 10**

“Palikuwa na mtu Kaisaria, jina lake Kornelio, akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia, mtu mtauwa,**mchaji** wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi, na kumwomba Mungu daima…... “

**Mwanzo 22:20-33**

“ Ndipo malaika wa Bwana akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa. Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa **unamcha** Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, mwanao wa pekee. “

**Ayubu 1**

“Palikuwa na mtu katika nchi ya Usi, jina lake alikuwa akiitwa Ayubu; mtu huyo alikuwa mkamilifu na mwelekevu, ni mmoja **aliyemcha** Mungu, na kuepukana na uovu. “

“**Yohane 14.15**

Mkinipenda, mtazishika amri zangu. “ ukisema unapenda Yesu uwe umeshika amri zake kwa kuzitenda siyo kwa maneno ya kinywa tu. Kushika amri za mungu kunakupa uzima iko afya ya mwili wako.

# 9.RUSHWA

Ni kitendo cha kutoa au kupokea mlungula ili uhudumiwe isivyo haki au utoe huduma isivyo haki. Mfano Ee mtu wa kimataifa uliyeoka fikiri wewe u mwalimu ktk shule za kimataifa pengine mwanafuzi unayemfundisha kafeli somo lako unakupa shs mil 7 umwongezee maksi ktk somo lako ukikubali hiyo ndiyo rushwa unapaswa kukataa hata kama unalipwa shs mil 2 kwa mwezi pengine hatoshi kwa mahitaji yako.

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka rushwa ni dhambi  tena unaweza kukutana nayo kazini au ktk biashara zako ikatae maana ni chukizo kwa Bwana Yesu.

Rushwa uharibu ufahamu kadri unavyoipokea ndivyo ufahamu wako unavyozidi kuharibika. Uwezo wa ufahamu wako kufikiri kupata kipato unachopata kwa kupokea rushwa kwa mfano kwa mwezi bila kuipokea hudumaa ndio kuharibika kwa ufahamu.

Jinsi ya kuacha rushwa ni kukataa kuipokea na kutosheka na mshahara pamoja na kuweza kwa haki ktk biashara unaweza kuanzisha bila kukopa na kutotaka kunia makuu kupita ulicho nacho kwa wakati huo. Mfano unalipwa mil2 pengine ktk matumizi yako unaweza kutumia mil.1 na kuweka mil.1 hivyo unaweza kufungua biashara ya mil.1 au ukaa miezi 7 unakuwa mil7. unaweza kufungua biashara mil7 kama butcher au duka.

**Luk 3.14**

“**Askari** nao wakamwuliza, wakisema, Sisi nasi tufanye nini? Akawaambia, Msidhulumu mtu, wala msishitaki kwa uongo; tena **mtoshewe** na **mshahara** wenu. “

Kushinda  dhambi ya **rushwa** ni **kutosheka** na **mshahara** wako  kama huna **mwombe** mungu aliye**mtoshelevu** kuumba hali ya kutosheka na mshahara wako na **kutosheleza** mahitaji yako na kukuepusha na rushwa.

# 10. ZINAA

Zinaa ni kufanya tendo la kinyume cha Amri za mungu kama usizini; yanayofanania usifanye uasherati ,usibake,usifanye ushugamami,usifanye ushoga au usifanye ufiraji .

Kwa nini zinaa? Ee mtu wa kimataifa ukweli ktk kazi za kimataifa utakutana mwanamke mwenye mitego kwa sababu ya kwenda nchi hata nchi ukweli ni walimbwende utakaofanya nao kazi kwa karibu usinaswe kwa sababu ya mavazi yao uzuri wao wa nje unaotoka na vipodozi kutokana na kukataa asili ya kuumbwa kwao.

**Mhubiri 7: 26**

"Nami nimeona lililo na uchungu kupita mauti; yaani, mwanamke ambaye moyo wake ni **mitego** na **tanzi**, na mikono yake ni kama vifungo; yeye ampendezaye Mungu atamponyoka, bali **mwenye dhambi atanaswa** na yeye. "

Ni aibu kwa uliyeokoka mtu wa kimataifa kunaswa naye maana wewe ni mwenye haki kwa Yesu. Hivyo kuomba mungu akuepusha na mwanamke mwenye mitego ni lazima maana unaweza kukutana naye ktk mazingira yako ya kazi.

Kama ni Mfanyabiashara wa kimataifa anawezekana mfanyabiashara mwenzako au mhudumu wa hoteli wa nchi unapeleka biashara zako.Njia ya kuacha au kukataa zinaa zinaweza kukupa ushindi ni kama zifuatazo :

- Kufunga kuzidi haki ya Farisayo aliyekuwa akifunga mara mbili kwa juma au siku mbili ktk juma.
- Kukimbia 1kor 6:18 & 1kor 3:16-17
- Jiepushe na matumizi ya chakula cha protini kupita kiasi wewe ni mtu mwenye elimu ee mtu wa kimataifa kama una masikio ya kusikia na usikie.

# 11. ANASA

Anasa ni starehe iliyochanyikana dhambi.Mfano Pombe na uzinzi,magomvi au sigareti,Disko na uzinzi au bangi au madawa yakulevya, Beach na uzinzi au pombe. Anasa kama kutoshika sabato yaani kuzifanya siku ya sabato au siku ya saba ya kukusanyika kwawaliokoka (Jumapili) siku za kupumzika ktk juma. Anasa ni chukizo kwa Bwana Yesu ewe mtu wa kimataifa kama ulikuwa na tabia kufanya anasa mwisho wa wiki kutokana na kuwa kazini ktk siku tano au sita acha na kataa anasa.

Njia ya kukataa au kuacha anasa baada kuokoka ee mtu wa kimataifa ni:=>

- Kuepuka kushirikiana maraki wa kwanza ktk kutenda anasa.
- Kutangaza wokovu kwa maraki zako wenye dhambi.
- Kujifunza starehe za haki alizokupa mungu na kujizoeza mwili kuzipenda kutafuta watu waliokoka wa kustarehe nao mwisho wa juma hasa jumamosi mfano kula na kunywa,kusoma vitabu na magazeti ya injili,kutazama vipindi vya video za injili ,Kutazama nyimbo za waimbaji wa injili,kusikiliza vipindi vya injili ktk redio za injili.
- Muda uliokuwa unautumia kwa anasa utoe kwa mungu kwa maombi (Yawezekana hata binafsi)au ibada).

**Luk 8.14** “Na zilizoanguka penye miiba ni wale waliosikia, na katika kuenenda kwao husongwa na shughuli na mali, na anasa za maisha haya, wasiivishe lo lote. “

Ktk wokovu wako ukipenda anasa kutokana kurudi nyumba yale mafundisho ya yesu utakayofundishwa hayatabadilisha matendo ya maisha yako na kuwa na nuru. Basi nuru iliyomo ndani yako ikiwa giza si giza hilo.

## 12. ULAFI

Ulafi ni kupenda kula kupita kiasi. Kwa kawaida mtu hula mara tatu kwa siku kwa kitanzania na mara nne kwa siku kwa kiingereza. Ulafi ni kula zaidi ya mara tatu au mara nne bila sababu ya msingi wakati mwingine vitu vidogo vidogo vya njiani visivyo vya lazima ktk siku .

**Luk 21.34**

"Basi, jiangalieni, mioyo yenu isije ikalemewa na **ulafi,** na ulevi, na masumbufu ya maisha haya; siku ile ikawajia ghafula, kama mtego unasavyo; "

Ukiwa **mlafi** ktk maisha yako ya wokovu kupokea ujio wa Mungu, Yesu , Roho mtakatifu au malaika aliyetumwa na mungu kukuletea ujumbe ni ngumu siyo rahisi. Kwa sababu siyo rahisi kukesha ktk maombi.

**Rumi 13.13 –14**

" Kama ilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa **ulafi** na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu.

Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake. "

Ee mtu wa kimataifa uliyeokoka uwe na adabu unapokusanyika kanisa au waliokoka wenzako usipende kula vyakula vya anasa yaani ulafi na utende uasherati kwa wanaume usiangalie mwili hata kuwasha kuwasha tamaa zake yaani hata aliyeokoka mwenzako sio jirani yako au kazini kwako au rafikiyo.

Mvae Bwana Yesu kwa kuwa kiasi ktk kula,hata kumwangalia mwanamke bila kuwasha tamaa. Mwombe Bwana Yesu akupe kiasi ktk mambo ya mambo ya mwili kama kula na tamaa ya mwili jifunze kufunga na kumzidi farisayo anayefunga mara mbili kwa juma siyo kuomba peke yake.

## 15. KUOKOKA

Kama hujaokoka ewe mtu wa kimataifa na unataka kuokoka kiri maneno yafuatayo kwa kinywa chako kwa Imani Sema,

"Bwana yesu ninakuja kwako mimi ni mwenye dhambi natubu naamini ya kwamba ulisulubiwa kwa ajili ya dhambi zangu na laana zake damu yako ilimwagika nipate ondoleo la dhambi na kupatanishwa na baba yako na ulipigwa nipate ondolewa dhambi zangu, nisamehe dhambi zangu na uniondolee bila kusahau laana zake na ulifufuka nipewe maisha mapya huru mbali na dhambi na laana zake yaani maisha ya haki na baraka Yesu ingia ktk maisha yangu na ufalme wa mungu pamoja na roho mtakatifu unipe maisha hayo ya haki yako na baraka zake pia.Andika jina langu mbinguni nijaze furaha yako ya kunisamehe na kuniondolea dhambi na laana yake na kufanyika mwana mbinguni na kupewa sehemu ya urithi wako wa kutembea na nguvu na mamlaka ya mungu wako ya kuzivunja na kuziharibu kazi za shetani ikiwepo mapepo,magonjwa n.k. Asante yesu kwa kuniokoa , kwa roho mtakatifu, kwa neema yako, kwa karama au vipawa vyako, mamlaka yako, ufalme wako na nuru yako maana umeyafanya maisha yangu kuwa na uzima wako ... Amen"

Sasa umeokoka tafuta kanisa au huduma ya waliokoka na ushirikiane nao ili upate kukua hata kufikia ufahamu wa cheo cha kristo yaliyo ktk nchi yako au bara lako lakini kama upo Tanzania karibu efatha church yapo makanisa au huduma zingine za waliokoka au Ben Hinny ministry kama upo Marekani ; Paula white ministry n.k Yesu akuongoze kwa Roho wake mtakatifu kukupeleka ktk kanisa au huduma ya waliokoka ambayo utakuwa kufikia ufahamu wa cheo cha kristo ili Yesu akutumie sawa na kusudi lake la kukuokoa.

## 16. MWISHO

Kitabu cha kuokoka kwa **mtu wa kimataifa** kipo kukupa ufahamu wa yesu uliyempokea alichokutendea yeye na Baba yake wa mbinguni mpende kwa kulitii neno lake mfano **mafundisho yake** na **nabii zake .**


Ukitaka kuwasiliana na Mtumishi ya Yesu Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister :

**Tovuti:** www.mhubiriwakimaifa.org

**Baruapepe:** listlameck5@gmail.com

**Simu:** +2550658601034 or 0658601034

**Sanduku la Barua:** Efatha Church: P.o Box 35666

Mwenge DSM Tanzania



Mhubiri wa kimataifa Lameck Lister niliokoka mwaka 2003 kwa kuongozwa sala ya kuokoka na Paul Roberty nilipokuwa kidato cha Tatu Kibaha Sekondari nikiwa na umri wa miaka 17 ndipo nilipoupokea ufalme wa mungu.

**Mafundisho ya kukulia wokovu na Ubatizo wa maji mengi**

Mafundisho ya kukulia wokovu na ubatizo niliyapata ktk kanisa la Efatha mwaka 2003-2006. Yanahusu maisha mapya ya mtu aliyeokoka anavyotakiwa kuishi na ubatizo wa kristo. Ndani ya hayo mafundisho yanazungumzia maisha ya toba. tofauti ya maisha kabla hujaokoka na baada ya kuokoka na kile Yesu na baba yake amefanya ndani ya mtu aliyeokoka.

**Mafundisho ya Roho mtakatifu**

Mafundisho ya roho mtakatifu niliyapata mwaka 2007 ktk kanisa la Efatha - Mwenge DSM Tanzania. Na kuwekewa mkono na Mtume na Nabii Josephat . E. Mwingira mkuu na mwanzilishi wa kanisa la Efatha ili kujaa roho mtakatifu kwa upya na vipawa au karama kama ilivyo neema ya Mitume itokayo kwa Yesu kristo.

**Utumishi wa mungu**

Baada ya kumaliza mafundisho yote nimepewa cheti cha utumishi wa mungu cha ufahamu wa cheo cha kristo. Natambulikana ndani ya kanisa la Efatha kama Mtumishishi wa mungu mbele baba yake Yesu na Yesu kama mhubiri wa kimataifa. Ukitaka kuona cheti cha utumishi wa mungu nilichopata Ktk Kanisa la Efatha

Website:www.mhubiriwakimataifa.com

Email:listlameck5@gmail.com

Mobile: +255658601034 ; 0658601034